## 1.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI 2016/17.

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara katika Mwaka wa fedha 2016/17, Serikali Kuu iliidhinisha jumla ya Tshs. **Tshs. 32,198,167.00/=** kama ruzuku kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara. Kati ya hizo Tshs. **21,507,528.00/=** kwa ajili ya Mishahara (PE), Tshs **Tshs. 2,309,303.00/=** kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), Tshs. **2,392,467.00/=** Mapato ya vyanzo vya ndani na Tshs. **5,988,869.00/=** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Hadi kufikia Mwezi Juni, 2017 Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ilikuwa imepokea Jumla ya Tshs. **32,033,641,398.21/=** ikiwa in asilimia **72.2%** ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mgawanyo ufuatao; Tshs. **22,082,581,375/=** kwa ajili ya Mishahara (PE), Tshs.**767, 527,082/=** Ruzuku ya matumizi mengineyo (OC), Tshs. **1,508,267,005.21/=** Mapato ya vyanzo vya ndani na Tshs **5,144,797,587.21** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI 2017/18.

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya **Tshs. 36,684,055.00/=** kwa mchanganuo ufuatao; Ruzuku ya Mishahara (PE) Tshs.**24,635,957.00,** Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC) Tshs. **1,225,949.00** Makusanyo ya ndani Tshs**. 2,469,275.00.** Miradi ya Maendeleo Tshs.**8,352,874.00**

Hadi kufikia Mwezi Desemba 2017, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ilikuwa imekusanya jumla ya Tshs. **15,498,081,000** sawa na **42** mchanganuo wa mapato hayo ni kama ifuatavyo;**Tshs.** 11,126,578,000.00**/=** ikiwa ni Ruzuku ya mishahara,**Tshs. 581,982,000/=** ikiwa ni Ruzuku ya Matumizi mengineyo, Tshs. **694,657,000/=** ni mapato ya vyanzo vya ndani na Tshs. **3,094,864,864/=** ni Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo.